UrithiWETU

MITI ILIYOGEUKA MAWE

Almasi mpya ya utalii kusini mwa Tanzania

Mhifadhi wa Pori la akiba Liparamba na msimamizi wa kisiwa cha Lundo, Maajabu Mbogo akitoa maelezo kwa Miss Utalii Ruvuma kuhusu miti jamii ya mitetereka inayogeuka kuwa mawe ambayo inapatikana kwa wingi katika pori la Akiba Liparamba.

Miti ya mitetereka katika msitu wa Kijiji cha Mbati wilayani Tunduru ushoroba wa Selous -Niassa.







Na Albano Midelo

WAKATI dunia ikihangaika kusaka vivutio vipya vya utalii vinavyoweza kuvutia watafiti, wapenda historia na watalii wa kawaida, Mkoa wa Ruvuma una siri nzito iliyolala kwa mamilioni ya miaka; miti iliyogeuka mawe.

Ndani ya ushoroba mkubwa wa Selous–Niassa na Pori la Akiba Liparamba, historia ya jiolojia imehifadhiwa kama maktaba hai ambayo bado haijasomwa vya kutosha.

Vivutio hivi adimu vinatajwa na wataalamu kuwa miongoni mwa hazina chache Afrika na vinaweza kuiingizia Tanzania mapato makubwa ya kigeni, iwapo vitaendelezwa na kutangazwa kimataifa kwa kiwango cha kutosha.

Utajiri usiosimuliwa wa Selous– Niassa

Ushoroba wa Selous– Niassa, moja ya maeneo yenye mfumo mkubwa wa ikolojia barani Afrika, kwa muda mrefu umejulikana kwa makundi makubwa ya wanyamapori kama tembo, swala, nyati na simba.

Hata hivyo, nje ya upekee wa wanyamapori hao, utafiti wa kina uliofanywa na wataalamu kutoka nje ya nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii umebaini utajiri mwingine mkubwa wa aina zaidi ya 2,100 za mimea, ikiwemo aina 600 za miti adimu isiyopatikana sehemu nyingine duniani.

Ni katika utajiri huu ndipo siri ya miamba ya ajabu inayofanana na magogo ya miti ilipofichuka, magogo yaliyogeuka kuwa mawe kamili, kitaalamu yakijulikana kama ‘fossilized tree trunks’ (visukuku vya mashina ya mti).

Mahali ilipoganda historia

Wakazi wa vijiji vya Mpurakacheche na Mbarang’andu wilayani Namtumbo na eneo la Mbati wilayani Tunduru, wamekuwa wakiishi karibu na historia bila kuitambua. Ndani na nje ya maeneo ya hifadhi, mabaki ya miti hii ya mawe yamesambaa, kana kwamba wakati ulisimama na kuacha historia ikiwa ‘imerogwa’ katika jiwe.

Mkurugenzi Mstaafu wa Uhifadhi na Mwanzilishi wa Pori la Akiba Liparamba, Ngwatura Ndunguru aliyetumia muda wa zaidi ya robo karne kuchunguza hifadhi hizo, anasema miti hiyo ni mojawapo ya maajabu ambayo Tanzania bado haijayatangaza ipasavyo.

“Ni vigumu kuamini hadi uone. Matawi, mashina, hata sehemu zilizodondoka zinaonekana wazi katika mawe haya. Sayansi imethibitisha kuwa haya ni masalio ya miti, si mawe ya kawaida,” anasisitiza Ndunguru.

Inaendelea Uk. 10

Ngorongoro, jamii na ujirani mwema kushiriki uhifadhi



Waziri wa Maliasili na Utalii Dk Ashatu Kijaji akiwa na Menejimenti ya Mamlaka ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) alipotembelea Karatu hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu

NOVEMBA 28, 2025 Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Ashatu Kijaji alikuwa na mazungumzo na Menejimenti ya Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kama sehemu ya ziara ya kujitambulisha kwenye taasisi hiyo na kukagua utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

Katika mazungumzo hayo, Dk Kijaji anaelekeza taasisi za uhifadhi kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za wanyamapori ili kupunguza migongano kati ya binadamu na wanyamapori.

Anasema kila taasisi haina budi kuwekeza kwenye teknolojia za kisasa ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali hizo za nchi ambazo ni kichocheo na kivutio cha wageni mbalimbali kutembelea nchi na kuingiza fedha za kigeni.

Katika kikao hicho, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamad Hassan Chande anawataka watumishi katika sekta ya uhifadhi na utalii kufanya kazi kwa kuzingatia weledi na ubunifu katika kuhudumia wageni.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk Hassan Abbasi anasisitiza watumishi wa NCAA kuimarisha ushirikiano baina yao, uongozi wa wizara, jamii na serikali kwa ujumla ili kuharakisha mipango ya serikali katika kuimarisha uhifadhi inatekelezwa na kuzaa matunda bora zaidi.

Kisha, viongozi hao wanapata fursa ya kukagua ujenzi wa makao makuu ya mamlaka hiyo, sambamba na shughuli za utalii katika lango la Loduare na Makumbusho ya Kihistoria ya Urithi ya Jiopaki ya Ngorongoro (Urithi Geo Museum).

Hayo yanajiri siku chache baada ya wananchi wa Kitongoji cha Ormekeke katika Kijiji cha Nasipaoriong wilayani Ngorongoro kuanza kunufaika na mradi wa maji, baada ya serikali kupitia mamlaka hiyo kuchimba kisima chenye uwezo wa kuzalisha lita 13,00 kwa saa na kujenga tangi lenye uwezo wa kuhifadhi lita 135,000 za maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Ashatu Kijaji

Kimsingi, hatua hii inadhihirisha kuwapo uhusiano mwema wa kindugu baina ya wananchi (jamii) na NCAA katika kushughulikia changamoto za kijamii zilizopo, ikiwamo ya maji.

Akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo hivi karibuni, Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Abdul-Razaq Badru anasema kukamilika kwa mradi huo kumekuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wa maeneo ya Ormekeke, Nasipaoriong na Olduvai.

Kwa mujibu wa uzoefu wa vyanzo mbalimbali, wakati wa kiangazi, watu wa maeneo ya NCAA hulazimika kuhamishia mifugo katika maeneo mengine kufuata maji.

"Mradi huu tuliuanza kwa kuwashirikisha wananchi, ikiwa ni utekelezaji wa kuboresha mahusiano ya NCAA na jamii kwa kutatua changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo ambazo moja wapo ni hii ya maji," anasema Badru.

Anaongeza: "Umeshakamilika na watu wa Kitongoji cha Ormekeke wameanza kutumia maji. Rai yangu kwa wananchi ni kulinda na kusimamia miundombinu ya mradi huu, kupitia kamati za maji na mazingira ambazo wameshaziunda."

Msimamizi wa Mradi huo, Godlove Sengele anasema pamoja na kunufaisha wananchi na mifugo yao, mradi huo pia utahudumia Makumbusho ya Olduvai, Leakey Camp, Mtui Camp, nyumba za askari pamoja na jamii ambayo imejengewa vituo vinne vya kuchotea maji na vituo vitatu vya kunyweshea mifugo.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ormekeke, Oreteti Olenjorio anasema eneo la kitongoji hicho ni kame na hakina chanzo chochote cha maji, hivyo mradi huo ni wa manufaa makubwa na wanautazama kwa jicho la umakini wa kipekee.

Kwa msingi huo, anasema uamuzi wa serikali kupitia NCAA kuchimba maji ni msaada mkubwa kwa matumizi ya wananchi na mifugo.

Olenjorio anaahidi kushirikiana na wananchi kuhakikisha wanalinda miundombinu ya mradi huo kupitia jumuiya za watumiaji wa maji, huku pia wakizingatia sheria za hifadhi.

NCAA si tu kwamba inakazania uhifadhi na kusahau huduma za kijamii na ushirikishwaji wananchi, bali pia kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii inawashirikisha wanajamii katika mambo mbalimbali.

> Mradi huu tuliuanza kwa kuwashirikisha wananchi, ikiwa ni utekelezaji wa kuboresha mahusiano ya NCAA na jamii kwa kutatua changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo ambazo moja wapo ni hii ya maji.

Moja ya mambo hayo, mbali na hilo la kuwezesha upatikanaji wa huduma za maji kwa jamii, lingine ni la hivi karibuni la kuwezesha wanawake 84 kutoka Kata ya Ganako wilayani Karatu, kufanya ziara ya mafunzo ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Ziara hiyo inafanyika baada ya wanawake hao kupewa mafunzo ya kutengeneza majiko banifu ili yawasaidie katika juhudi zao na za taifa za kulinda mazingira, kwa kupunguza na kuepuka matumizi ya majiko yanayochochea uharibifu wa mazingira, kupitia ukataji miti kupata kuni na kuchoma mkaa.

Matumizi ya nishati safi ya kupikia ni ajenda mahususi inayochukua nafasi kubwa katika sera, mipango na mikakati ya serikali mbalimbali duniani. Umuhimu wa ajenda hii unasukumwa na ongezeko la uharibifu wa mazingira na athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi za kiafya.

Lengo Namba 7 la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa limejikita kuhakikisha kuna upatikanaji wa nishati nafuu, inayopatikana kwa urahisi, endelevu na ya kisasa kwa wote.



Kamishina wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Abdul-Razaq Badru.

Kwa mujibu wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034), zipo athari mbaya za matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia, zikiwamo za kiuchumi na kimazingira.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa NCAA, Lightness Kyambile anasema, ziara hiyo ni sehemu ya Programu ya Elimu kwa Vitendo inayolenga kuhamasisha uhifadhi wa mazingira na matumizi ya teknolojia rafiki, inayosaidia kuepuka ukataji miti hovyo unaolenga kupata kuni na mkaa kwa jamii inayozunguka Hifadhi ya Ngorongoro.

Lightness anasema hatua hiyo inalenga kuwezesha wanawake katika jamii hiyo kuwa mabalozi bora zaidi wa uhifadhi, kwa kuepuka kasumba ya kuharibu mazingira kupitia ukataji miti unaolenga kupata kuni na mkaa.

Wanawake walioshiriki ziara hiyo wanashukuru uongozi wa NCAA kwa kuwapa fursa ya kujifunza kwa vitendo masuala ya uhifadhi.

Wanaahidi kuendelea kutoa elimu hiyo kwa wanajamii wengine, wakiwamo wanawake wenzao katika vijiji vyao.

Ziara hiyo ya mafunzo imeandaliwa kwa kuwashirikisha Ganako Youth ambao wamekuwa mstari wa mbele kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, kama njia ya kulinda mazingira na kukabili athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi.

Almasi mpya ya utalii Kusini mwa Tanzania



Inatoka Uk. 9



Ruvuma katika ramani mpya ya utalii

Kwa mujibu wa wataalamu, mchakato wa kugeuka jiwe kwa miti hii ulitokea kwa zaidi ya miaka milioni iliyopita, kutokana na mabadiliko ya kijiolojia yaliyosababisha madini kama silika kupenya kwenye mashina ya miti na kuganda kama mawe halisi.

Kivutio kisichopatikana kwingine

Kulingana na mhifadhi, Deborah Emily anayesimamia masuala ya utalii katika Kanda ya Kusini, kivutio hiki ni adimu mno.

"Utafiti unaonesha kuwa, maeneo haya ya Ruvuma ndiyo pekee Kusini mwa Jangwa la Sahara yenye miti iliyojiweka katika umbo la jiwe. Huu ni utalii wa kipekee ambao nchi nyingine zinauhifadhi kama madini ya thamani," anasema.

Duniani kote, maeneo machache sana yana historia ya kijiolojia kama hii. Miongoni mwao ni Misri, Libya, Algeria, Ugiriki na baadhi ya maeneo ya Marekani, hususan Msitu wa Amazon. Tanzania kupitia Ruvuma inajiunga rasmi kwenye orodha hiyo ya mataifa yenye urithi wa milioni ya miaka.

Ardhi ambayo historia haijaguswa

Katika Pori la Akiba Liparamba, hali ya kuhifadhiwa kwa mawe haya ni ya kushangaza. Eneo hilo halikaliwi na watu, jambo lililosababisha maumbile ya miti mawe kubaki katika hali yake ya asili kwa karne nyingi, bila kuathiriwa na shughuli za kibinadamu.

Hii ndiyo sababu inayofanya wataalamu waamini kuwa, Liparamba inaweza kuwa kituo kikuu cha utalii wa kijiolojia nchini.

Msimamizi wa Pori la Akiba Liparamba na Hifadhi ya Kisiwa cha Lundo, Maajabu Mbogo anatoa maelezo zaidi kuhusu pori hilo.

"Katika Pori la Liparamba, miti jamii ya mtetereka inapokauka hugeuka jiwe halisi. Kuna mawe makubwa yenye uwezo mkubwa wa kuvutia watalii wanaopenda kupanda mawe. Aina hii ya utalii inapata umaarufu mkubwa duniani," anaeleza.

Fursa kubwa ya kiuchumi

Zaidi ya aina 600 ya miti adimu duniani inapatikana katika ushoroba wa Selous–Niassa. Aina 2,100 za mimea hiyo zimetambuliwa kisayansi.

Ruvuma ni eneo pekee Kusini mwa Sahara lenye miti iliyogeuka mawe na dunia ina maeneo machache sana yenye kivutio hiki, ni chini ya 10 yaliyotambuliwa rasmi.

Endapo utalii huu utaandaliwa kitaalamu, wataalamu wa uchumi wa maliasili wanakadiria kuwa unaweza kuongeza mapato ya mkoa kwa zaidi ya asilimia 30 ndani ya miaka minne, kutokana na ongezeko la watalii wa ndani na nje ya nchi.

Sera na wajibu wa Serikali

Kwa mujibu wa sera na sheria za usimamizi wa rasilimali za maliasili nchini, ikiwemo Sera ya Maliasili na Utalii (1998) na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya 2009, maeneo ya urithi wa kijiolojia kama haya yanapaswa kulindwa kwa kiwango cha juu ili yasiharibike.

Aidha, yanapaswa kuendelezwa kwa kuwekewa miundombinu rafiki kwa watalii, kutangazwa ndani na nje ya nchi, kuingizwa kwenye ramani za kitaifa za vivutio vya utalii na kutumiwa kama sehemu za tafiti za kitaalamu katika vyuo na taasisi za kimataifa.

Wataalamu wanasema kutangaza kivutio hicho pekee kunaweza kuifanya Ruvuma kuwa kitovu cha utalii wa kijiolojia Afrika Mashariki, ndani ya miaka michache.

Urithi uliolala ukisubiri kuamka

Mkoa wa Ruvuma umebarikiwa urithi ambao mataifa mengine yangeutangaza kwa gharama kubwa na kuugeuza kuwa kisima cha fedha.

Miti iliyogeuka mawe si tu kivutio cha kitalii, bali ni simulizi ya dunia, somo la kijiolojia, hazina ya kiuchumi na alama ya upekee wa Tanzania.

Ni wakati sahihi kwa wizara, wataalamu na sekta binafsi kushirikiana kuweka Mkoa wa Ruvuma kwenye ramani ya utalii wa dunia.

Kila jiwe lenye umbo la gogo ni shahidi wa historia na kila mtalii atakayekanyaga ardhi ya Selous–Niassa atakuwa shuhuda wa sehemu ya maajabu ya dunia kutoka Ruvuma, Tanzania.